

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO

06 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – TAREHE 06 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**380. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA
(BUKOBA VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Katika Bunge la Kumi kulikuwepo na mjadala kuhusu kuanzishwa kwa Kilimo cha Makambi ambapo vijana wengi wangepelekwa makambini, wangepewa mikopo ya pembejeo na kuzalisha mazao kwa wingi. Mazao hayo yangeuzwa nje ya nchi na vijana wengi wangejajiri. Aidha, mpango huo uliingizwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM):-

Je, ni lini makambi hayo yataanzishwa.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

381. MHESHIMIWA JANET ZEBEDAYO MBENE (ILEJE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

- (a) Je, mradi wa Tanzania na Malawi wa kujenga mabwawa matatu makubwa kandokando ya Mto Songwe umefikia wapi;
- (b) Mradi huo ulikuwa uanze kwa awamu tatu; na ya kwanza ilikuwa iwe Ileje lakini unaanzia Kyela kisha uende Malawi na kumaliza awamu ya tatu Ileje; Je, ni nini kilifanya utaratibu wa awali ubadilishwe;
- (c) Wananchi wa Kata za Bubigu na Ileje walishaambiwa wasifanye shughuli zozote katika eneo hilo ili kupisha mradi huo; Je, kuna mpango gani wa kuwalipa fidia au kuwaruhusu waendeleo na shughuli zao.

382. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kuna miradi ya umwagiliaji iliyogharimu fedha nyingi kuijenga lakini

inatumika chini ya uwezo na usanifu (*below designed capacity*) kwa sababu mbalimbali:-

(a) Je, ni Halmashauri ngapi zina fursa ya kilimo cha umwagiliaji na zimewekeza kwa kiwango cha kutosha kwenye miundombinu ya umwagiliaji;

(b) Je, kuna mpango wowote unaotekelezwa wa kuwapata wataalam wa umwagiliaji katika muda mfupi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

383. MHESHIMIWA HAMAD SALIM MAALIM (KOJANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Wavuvi wengi nchini wanaendesha shughuli zao za uvuvi kwa kutumia njia zisizokuwa za kitaalam:-

Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo ya kitaalamu kwa wavuvi wetu ili kuwawezesha kufanya kazi yao kwa ufanisi.

WIZARA YA NISHATI:

384. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini tatizo la kukatika mara kwa mara kwa umeme katika Mkoa wa Mtwara litaisha.

385. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Serikali iliahidi kuvipatia Vijiji vingi vya Jimbo la Mbulu Vijijini umeme wa REA III:-

Je, ni lini sasa umeme utafika katika Vijiji vya Endahargadat, Endahagichani, Qamtananat, Mewadan, Endalat, Gidbiyo na Manguhay.

386. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIA BUKWIMBA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-
Lengo la Serikali ni kuhakikisha kila Kijiji kinapata umeme wa REA:-

Je, ni lini sasa Vijiji vyote vya Jimbo la Busanda vitapata umeme.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

387. MHESHIMIWA OSCAR RWEASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wananchi wa Kijiji cha Luganzu na majirani zao wa Ntumagu wanakabiliwa na adha kubwa ya matukio ya ujambazi pamoja na ukosefu wa Kituo cha Polisi Kijijini hapo kwa ajili ya kuimarisha ulinzi:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hali hiyo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

388. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (BABATI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Vijiji vya Imbilili, Hitimi na Managha katika Jimbo la Babati Mjini havina mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini Serikali itavipatia Vijiji hivyo minara ya Mitandao ya simu.

389. MHESHIMIWA GOODLUCK ASAPH MLINGA (ULANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Ifakara mpaka Mahenge Mjini ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao kama Mpunga, Mahindi, Ufuta, Ndizi na Maharage:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

DODOMA
06 JUNI, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE